30.2 KISWAHILI (102)

30.2.1 Kiswahili Karatasi ya 1 (102/1)

MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

1. Umuhimu wa michezo na sanaa

   - Insha ifuate kanuni zote za utoaji wa hotuba. Pawe na mwanzo ambao unaweza kuwa ni salamu au wito wa kuhamasisha hadhira inayohutubiwa.

   - Waliofika watangulizwe kulingana na hadhi zao/vyeo vyao na utoaji wa lengo la hotuba ili kuvuta nadhari za hadhira.

   Sehemu ya kati: Utoaji wa ujumbe kwa kina na mapana na uwe ni wa kweli wala si porojo.

   Sehemu ya mwisho: Hotuba itoe changamoto kwa hadhira na kuipa matumaini. Hatimaye pawe na shukrani na kuaga/hitimisho.

   Hoja:

   1. Michezo huwezesha wahusika kuimarisha afya/siha na hivyo kuepukana na athari za magonjwa kama ule wa mshtuko wa moyo, shinikizo la damu nk.
   2. Huwaleta watu pamoja, wachezaji kwa hadhira. Mjumuiko huu husaidia kuondoa hisia hasi miongoni mwa wanajamii na hivyo kuleta utangamano wa kijamii.
   3. Hutoa nafasi ya kujiburudisha kwa wahusika na pia hadhira.
   4. Hutoa nafasi ya ajira kwa baadhi ya watu kama vile makocha, marefa, wachezaji, waandishi wa habari n.k
   5. Baadhi ya michezo kama vile michezo ya kuigiza, unyoshaji wa misuli huweza kuendeleza utamaduni wa jamii.
   6. Huwa ni nafasi bora ya kutumia wakati vyema hasa miongoni mwa vijana ambao wanaweza kujitumbukiza katika mambo yanayoweza kuwadhuru.
   7. Kuendeleza ubunifu baina ya wanamichezo/wasanii.

2. Madhara ya utalii
   - Utalii huambatana na ongezeko la uasherati
   - Maradhi ya kuambukiza nayo husagaa.
   - Katika maeneo ya utalii watoto huacha shule kwa wingi kutokana na biashara hii ya utalii.
   - Afyuni nazo huongezeka kupitia kwa watalii k.m. dawa za kulevya.
   - Bei ya baadhi ya bidhaa kupanda maradufu na hili jambo huwatatiza wengi.
   - Wananchi huzuiliwa kwenda katika baadhi ya maeneo kutokana na biashara hii.
   - Ongezeko la uhalifu/ughaidi
   - Maadili huvurugika
   - Utamaduni huathiriwa vibaya.

   Faida

   - Hutoa nafasi za ajira kwa wenyeji.
   - Nchi hupata hela za kigeni ambazo hutumiwa kuiendeleza nchi
   - Miundo msingi kama barabara, viwanja vya ndege n.k. huimarika

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Miji nayo hupanuka na kustawi.
- Wakulima na wenye biashara zinasohusiana na utalii hufaidika.
- Mtagusano hupanua utamaduni kwa njia nzuri.

3. Samaki huanza kuoza kichwani
   - Mtahiniwa aandike kisa kimoja ambacho kinadhihirisha kuwa asasi yoyote ya kijamii ambayo imepotoka, huanzia kwa viongozi wake. K.m. Iwapo watoto hawana maadili, wazazi ndio waliotangulia kuyakosa.

4.
- Hii ni insha ya mdokezo. Insha hii inarejelea kuonyesha namna vijana walivyotengwa na
- kunyimwa nafasi ya kujiendeleza katika familia na jamii kwa jumla. Vijana wengi
- wamepata elimu ya juu ilhali hawana nafasi za kupata riziki.
- Wengine wameingilia matumizi ya afyuni ilhali jamii haifanyi juhudi madhubuti za kukabiliana na suala hili.
- Vijana wengine nao wamekabwa na tamaduni kongwe ambazo zinawanyima nafasi za kujiendeleza na kujipatia riziki.
- Asasi za familia ambazo zinatakiwa kutoa nasaha kwa vijana nazo zimeporomoka na hawapati ushauri huu.

*Mambo haya yote yakijumuishwa kwa pamoja yanaleta hali ambapo vijana wanalinganishwa na bomu linaloweza kulipuka wakati wowote; kwa sababu wao wana nishati ambayo lazima itumike kwa njia ipasayo.

*Kulipuka kwake ni vijana kutumiwa kuzua na kuendeleza fujo na ghasia kama ilivyoonekana nchini Ufaransa na nchini Kenya baada ya uchaguzi wa Desemba 2007.

30.2.2 Kiswahili Karatasi ya 2 (102/2)

1.0 **UFAHAMU**

a) Ung'amuzibwete hufanya kazi mtu anapokuwa usingizini/usiku ilhali ung'amuzi hufanya kazi mtu akiwa yu macho/mchana Alama 1 x 2 = 2

b) Mambo yanayopatikana katika ung'amuzibwete yana sifa hasi.
- Huficha/hubania mambo ambayo binadamu hawezi kuyasema (kadamnasi/wazi/peupe.)
- Hubania matamanio yasiyokubalika na jamii/makatazo ya jamii.
- Hubania kauli zilizoharamishwa na miko ya jamii. ***(Alama 3 x 1=3)***

c) Kwa ishara za ndoto
- Kwa mitelezo ya kauli
- Kwa ishara
- Kwa matumizi ya lugha ya kitamathali katika uandishi.

d) Freud aliuangalia ung'amuzibwete kama jaa la mawazo mabaya, fikra na dhana hasi ilhali Jung aliwaza kuwili.

AU
- Jung alizuka na ung'amuzibwete binafsi na ung'amuzibwete jumuishi

Powered By: www.manyamfranchise.com

AU

- Jung aliongezea ung'amuzibwete jumuishi

e) Ung'amuzibwete una uwezo wa kuathiri ung'amuzi na matendo ya binadamu ya king'amuzi.

(Hoja 1 x 2 =2)

2. **MUHTASARI**

a) Ni mshikamano wa hisia zinazowafungamanisha watu katika taifa.

- Kuwepo kwa mwelekeo mmoja
- Kuwepo kwa muono sawa/hatima sawa
- Umejengwa kwa hisia za mapenzi kwa nchi yake/uzalendo
- Hauna ubaguzi wa aina yoyote/hauna ukabila
- Kuwepo na falsafa/imani/itikadi sawa

b) Ni mwenye mapenzi makuu kwa nchi yake

- Hawezi kutenda mambo ya kuiletea nchi yake nakama/kuihujumu.

  AU
- Matendo yake huangazwa na mwenge wa mema anayoitakia nchi yake.
- Hawezi kutawaliwa na kitiba cha ubinafsi au umero wa kujilimbikizia mali.
- Matendo yake huongozwa na mwelekeo wa kutaka kuiboresha nchi yake.
- Yuko tayari kuhasirika kwa manufaa ya nchi/taifa lake.
- Hana taasubi za kikabila.

***Kutuza**

- Tuza alama 6 katika maudhui ya kisehemu cha (a)
- Tuza alama 6 katika maudhui ya kisehemu cha (b)
- Tuza alama 3 kwa utiririko mwanana katika maudhui.

***Kuadhibu**

- Ondoa alama 3 kwa makosa 6 ya mwanzo ya kisarufi.
- Ondoa alama 3 kwa makosa 6 ya mwanzo ya hijai/tahajia
- Ondoa alama 1 kwa kila ziada ya maneno 10 ya mwanzo kisha endelea kuondoa ½ alama kwa kila ziada ya maneno 5 hadi mwisho wa jibu la mtahiniwa.

***Mtindo wa kutuza**



a - 6

b - 6

u - 3

Jumla - 15

Ondoa – z na h/s

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

a) Duka la Bahati ambako/mo/po Juma anafanya kazi lina bidhaa nyingi

- Duka la Bahati anamo/ko/po fanya kazi Juma lina bidhaa nyingi.
- Duka la Bahati lenye bidhaa nyingi ndipo/lo/mo Juma anamo/po/ko/fanya kazi.

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Juma anafanya kazi katika duka la Bahati lililo/mlimo/palipo/kuliko na bidhaa nyingi
- Juma anafanya kazi katika duka la Bahati ambalo lina bidhaa nyingi.
- Katika duka la Bahati lililo na bidhaa nyingi ndimo/po/ko Juma anafanyakazi
- Katika duka la Bahati ambalo lina bidhaa nyingi ndipo/ko/mo Juma anamo/po/ko fanya kazi.

(Hoja 1 x 2=2)

b) (i)

- Kiambishi ngeli – LI-YA k.m Jina - majina
- Kujirejelea/kirejeshi
- Kuonyesha uzoefu.
- Kuonyesha ukubwa
- Kuonyesha udogo/udunishaji. ***(Hoja 2x1=2)***

(ii) **Mifano kwa kila matumizi**

Ngeli - Jicho lake linauma
Kujirejelea - Mtoto anajifunza kujilisha
Ukubwa - Jitu hili ndilo litishalo mno
Udogo - Kijirembo kile kimerembeka ajabu
Uzoefu - Juma ni mwimbaji hodari

(Alama 1 x 2 =2)

c) <u>Visawe vya</u>

- Ukuta - Kiambaza
  -Sera
- Mvulana - Mvuli
  - Shababi (u)
  - Ghulamu
- Akiuparaga - Akikipanda (kiambaza) Akiipanda (sera)
  - Akikikwea (kiambaza) Akiikwea (sera)
  - Akikisombera (kiambaza) akiisombera (sera)
  - Akikiparamia (kiambaza) Akiiparamia (sera)

*Mtahiniwa avitumie visawe hivi kuiandika sentensi upya akizingatia upatanishi mwafaka.

(Hoja 3 x 1 = 3)

Powered By: www.manyamfranchise.com

d)



(Hoja 4x1=4)

c) M, gh

(Hoja 2x½=1)

f) Hufa (pia minyambuliko yoyote ambayo inaonyesha mazoea k.v – hufisha, hufiwa n.k.)
Mfano wa sentensi: Mvuta sigara hufa polepole.

(Alama 1 x2=2)

g) i) Malaika
ii) Nge pia 'Nge.

h) Maana

- Kiharusi – Aina ya ugonjwa
  - Harusi ndogo
  } Maelezo yajidhihirishe katika maana hizi
- Ugonjwa huu umewatia hofu watu wengine asipokuwemo.
- Ugonjwa huu umewatia hofu watu wengine na yeye akiwemo
- Harusi hiyo imewatia hofu watu wengine asipokuwemo
- Harusi hiyo ndogo imewatia hofu watu wengine na yeye akiwemo.

(Alama 2x1=2)

i)

- Kiganda
- Kiuganda

Alama – jibu moja
Sahihi – 1x2=2

Powered By: www.manyamfranchise.com

j)

- Hamali ameugua
- Hamali alisema
- Hamali angekwenda hospitali jana

(Alama 3 x 1=3)

k)

- Dovu la kiafrika limeharibu chaka

au

- Jidovu la Kiafrika limeharibu jichaka

(Alama 2x1=2)

l) Wachezaji watashinda mchezo wa leo

(Alama 2x1=2)

m) "Mtapenda kwenda Mombasa wakati wa likizo?"
Baba alituuliza. "Tunataka kwenda Kisumu kwa kuwa hatujaliona Ziwa Victoria."

AU

- Baba aliuliza, "Mtapenda kwenda Mombasa wakati wa likizo?" "Tunataka kwenda Kisumu kwa kuwa hatujaliona Ziwa Victoria." Tulimjibu. ***(Alama 1x3=3)***

n) Kuonyesha kosa la hijai/maendelezo mabaya.

- Kuonyesha kosa la sarufi
- Kuashiria ufafanuzi au maelezo yaliyotolewa chini baada ya maandishi makuu.
- Matumizi ya neno geni/lugha tofauti.
- Kuonyesha tahadhari.

(Alama 1x4=4)

0) Hapo napo sipo nitakapo.

AU

- Hapo napo ndipo nisipotaka/nisipopataka

(Alama 1x1=1)

p)

- Furaha amchama mashambani/kijijini
- Furaha amchama mjini ***(Alama 1x1=1)***

q)

- Imbisha
- Chokea

(Alama 2x1=2)

4. **ISIMUJAMII**

a) **Kiswahili Kama Lugha Ya Kitaifa**

- Hifadhi ya amali na utamaduni na ustaarabu wa taifa zima
- Hifadhi ya kumbukumbu za kihistoria
- Hukomesha/husitisha ukabila
- Kitambulishi cha watu wa Afrika Mashariki

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Ni ugwe wa kuunganishia watu katika taifa
- Huwapa watu hadhi na staha
- Hutumika katika utafiti
- Hutumika katika shughuli za
- biashara
- siasa
- elimu
- bungeni
- sheria/mahakama
- Sera
- Kidini
- Ni kitambulisho cha utaifa/hadhi na staha miongoni mwa mataifa mengine
- Ni chombo cha
  - utangazaji
  - Ajira
  - Burudani
  - Sanaa
  - Mawasiliano
  - Umoja wa kitaifa
- Ni kigezo cha kuchujia wanaojiunga na vitengo mbalimbali.
- Hukuza uzalendo
- Hutumiwa katika uandishi/uchapishaji
- Hutumika katika sherehe za kitaifa.

(Hoja zozote 5x1=5)

b) <u>Kama Lugha Ya Kimataifa</u>

- Ni lugha ya kufunzia vyuoni
- Ni chombo cha mawasiliano katika mikutano ya kimataifa
- Hutumika katika idhaa/kutangazia
- Hutumika katika uandishi/magazeti/majarida
- Hutumika kama chombo cha ajira k.m. B.B.C, VOA, Radio Uchina n.k.
- Kuandikia na kutafsiria maandishi/sanaa n.k.
- Kufanyia utafiti
- Kusambazia/kukuzia utamaduni wa mwafrika.
- Hutumika katika burudani
- Hukuza lugha zingine za kimataifa k.v. Kiingereza, Kichina, Kirusi n.k.
- Hutumika katika kukuzia
  - michezo
  - biashara
- Hukuza amani
- Ni kitambulisho cha utaifa
- Husawazisha watu wa mataifa mbalimbali
- Hutumika katika sherehe za kimataifa
- Hutumika katika teknolojia ya mawasiliano (teknohama)

(Hoja Zozote 5 x 1=5)

Powered By: www.manyamfranchise.com

30.2.3 Kiswahili Karatasi ya 3 (102/3)

a)

- Haya ni maelezo ya mwandishi kuhusu mawazo ya Selume;
- Anahisi hana mume kwani Shoka amepuuza wajibu wake
- Kama si wanawe, Selume hangejisumbua kutafuta chakula
- Anahisi hana mume kwani shika amepuuza wajibu wake
- Amemwachia jukumu la malezi na kutafuta riziki, kazi ya Shoka ni kudowea alichokitafuta Selume.

(4x1= alama 4)

b) Sitiari/Jazanda:Mifano:Shimiri za baruti — alama 1
Kutaja — alama 1
Mfano — alama 1

Maelezo:
→Matatizo ya ndoa na maisha ya Selume yanafananishwa na "Shimiri za baruti zanazoshindiliwa moyoni."
Matatizo hayoo yanamqumiza moyoni ***(Alama 2)***

(1) Msemo: nahua
Mfano:Kutanga na njia
Maelezo:-hangaika akitafuta, enda huku na huko.
(2) Nidaa/siyahi Lo! katu. Kuonyesha hisia za kuchukizwa na mkondo wa ndoa yake.

(c)

- Kudhulumiwa kwa mwanamke katika ndoa mf .Selume na Shoka.
- Kutowajibika kwa wanaume mf. Shoka
- Wanawake kuendelea kubaki katika ndoa za matatizo kwa sababu ya watoto wao na kujitolea kuteketeza yaliyopuuzwa na waume zao. ***(Zozote 2 x 2=4.)***

(d) (1)

- Asasi ya ndoa /unyumba – ya Maksuudi na Tamima na ya Maksuudi na Mwanasururu
- Matatizo kati ya mume na mke
- Dhiki zinazowakumba wanawake katika ndoa
- Tamima analazimika kutawa kwa amri ya mumewe Bw. Maksuudi
- Hana ruhusa ya kutoka wala kumwalika mtu nyumbani.
- Analazimika kujifungua nyumbani licha ya ushauri wa madaktari kutokana na msimamo wa mumewe.
- Bi Farashuu anapomsaidia kujifungua anacharazwa vibaya na mumewe na kufukuzwa nyumbani.
- Ananyimwa uhuru wa kuwa na mwanawe mdogo anayeishia kufariki
- Tabia ya Bw. Maksuudi inaishia kuivunja jamaa yao.
- Bw. Maksuudi anamwacha mkewe na kuwafuata wanawake wengine kama Shoka anavyomwacha mkewe na kufuata wanawake wengine huko nje.
- Mwanamke ananyimwa uhuru wa kuishi kama kiumbe anayeweza kujiamulia.
- Mwanamke hana uhuru wa kiuchumi → mf. Mwanasururu ananyimwa urithi wake.

(2). Utengano wa kijinsia/utengano kati ya wanawake na wanaume/mgogoro wa kijinsia/Taasubi ya kiume.

(i) Wanaweke wanatumiwa kama vyombo vya starehe mf. Kazija na Maksuudi, Shoka na Maimumna.

Powered By: www.manyamfranchise.com

(ii) Uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume unatawaliwa na chuki na kisasi → Biti Kocho/Farashuu na Maksuudi,/Kazija na Maksuudi.

(iii) Bi Tamima anateswa na Maksuudi hataki kumsamehe na kumrudia anapomtaka kufanya hivyo.

(iv) Uhusiano wa Maimuna na Bw. Maksuudi babake unaonyesha chuki inayotokana na matendo ya Maksuudi mwenyewe.

(v) Kazija anapanga njama ya kumfumanisha Maksuudi na mwanawe Mussa.

(3). **Ukatili**

(i) Maksuudi anavyomtendea Bi Tamima – kumtawisha
(ii) Maksuudi anavyomtendea Mwanasururu …
(iii) Maksuudi kumpiga na kumtaliki Tamima ilhali ana mimba bichi

(4). **Dhiki/Kudhulumiwa kwa Wanawake**

(i) Maksuudi kuwatawisha Bi. Tamima na Maimuna
(ii) Kumwendea kinyume Tamima (jicho la nje).
(iii) Maksuudi kumpora Mwanasururu mali yake.
(iv) Wanawake kuachwa nyuma kielimu na kikazi.

(5). **Nafasi ya Mwanamke katika jamii**

(i) Kuishi maisha ya kutawishwa mf. Tamima
(ii) Kufanya kazi duni mf. Ukahaba, uuzaji wa pombe haramu.

(6). **Umaskini**

(i) Wanawake kujihusisha na ukahaba ili wajikimu.
(ii) Wahusika wengine waliishi katika makazi duni: Biti Sururu, Jeni, Farashuu.

Maudhui yoyote mawili
Kutaja – alama 1
Maelezo – alama 3

(4 x 2 = Jumla — alama 8)

2. (a) Maisha ya wafanyakazi na vibarua shambani ni duni na ilhali wanaofaidika ni wengine. ***(Alama 2)***

(b) (i) Tabdila – mvuwa, kibaruwa
(ii) Lahaja – mte, kutipuza, mtilizi
(iii) Mazida – tisiya
(iv) Inkisari – ikajinamiya/lingiapo
(v) Kuboronga sarufi.

Kutaja 1, mfano 1 – zozote 2 x 2=4

(c) 1. **Tamathali:**

i) Tashhisi - ndege watumbuizao
Uhaishaji/ Uhuishi - upepo uvumao kwa ghadhabu
— Mito itiririkayo kwa furaha
ii) Ritifaa — waulize ndege kwa nyimbo
— iulize na mito
iii) Taswira — maji itiririkao
— upepo mkali kwa ghadhabu uvumao
iv) Takriri — Iulize, waulize, uulize

Kutaja – alama 1
Kueleza alama 1
Mbinu yoyote 1 x2 2

Powered By: www.manyamfranchise.com

2. **Mbinu ya kimuundo:**

i) Usambamba/Takriri —Urudiaji kimuundo
ii) Kina cha mwisho ni O/kipande 1
iii) Mizani ni sawa katika kila mshororo - 19
iv) Utatu/Tathlitha – mishororo mitatu
Mfana 1 Kutaja – alama 1
Kueleza – alama 1

(alama 2)

(d) i) Jasho la vibarua linafaidi wengine
ii) Wale wanaonyonya vibarua wajue kwamba wanafanya lililostahili.
iii) Vibarua wenyewe wazinduke (mshairi anauliza maswali ya kuchochea, ya kutafuta mwelekeo)
iv) Jamii nayo ijue vibarua wananyonywa.
v) Wanaotarajiwa kushughulikia haki za vibarua hawajali
vi) Vibarua wanafanyishwa kazi nyingi kwa malipo duni
vii) Wanadharauliwa na kutukanwa. ***(Hoja zozote 2 x2=4)***

(e) Swali ni kwamba ni nani anayelima na kupalilia mashamba? Mimea inayopatikana kwa wingi shambani ikazaa kwa wingi kutokana na juhudi za mkulima ambaye ni kibarua. Mwishowe ni nani anayepata utajiri wa mali hiyo yote akajilimbikizia, akanona na kuwa kama ana mimba hata akaongeza magari na kujipatia starehe kama kuwabadilisha wanawake. Swali hili liulizwe ili kubainisha ni nani hasa anayefanya kazi hiyo. ***(alama 4)***

(f) Kibarua manamba ni jina la :
i) tajiri au mwenye shamba
ii) mfanyikazi shambani (Tazama matumizi ya herufi kubwa)

(1 x 2 = 3)

3. (a) (i) Tendo litendwe kwa hekima kulingana na kauli tunazotoa.
(ii) Ukitenda la faraja utafaidika
(iii) Mtu anayetoa kauli au kutenda mabaya anajiletea maangamizi au kujivunjia heshima.
(iv) Mtu humfunza mwana ndipo mwana awe na heshima ili yeye kama mzazi asilaumiwe.
(v) Ni vyema kutenda mema ndipo mtu hupata heshima na baraka
(vi) Ni vyema kubainisha matendo mazuri na maovu.

(Zozote 4 x 1 = 4)

(b) (i) Mtu binafsi →kauli zenye upendo humfurahisha mtu binafsi.
→kalima yenye upendo kufurahisha mtima (ubeti 1)
(ii) Jamii→kuonyana na kuelekezana ni muhimu.
(iii) Mtoto→ni jukumu la mzazi kumfunza mtoto wake maadili.
→mtu hufunza mwanawe, kwanza ajue heshima (ubeti 4)
iv) Mzazi →nisipokwambia wewe,hukufunza kila jema (ubeti 5)
Kutaja – alama 1
Mfano – alama 1

(Hoja 3 x 2 = 6)

(c) i) Kama kimilizio cha ubeti
Msisitizo/ukariri wa ujumbe wa mshairi au kama dhamiri yake
ii) Mtu binafsi, jamii, mzazi au watoto wasipotenda mema, watapatwa na athari ya maovu yao. ***(Hoja 2 x 2 = 4)***

Powered By: www.manyamfranchise.com

(d) Mzazi asipomfunza mwanawe maadili/ambayo yatamwepusha na matatizo mbalimbali/huenda akalaumiwa na jamii/Hata hivyo mtu anayetenda maovu atajiingiza matatizoni kutokana na matendo yake ***(alama 4)***

(e) i) afuwaja – wavamizi, washambulizi

ii) taaluma – wasia/mawaidha/mbinu za kukabiliana na mambo, mafunzo,ushauri, elimu. ***(2 x1 = 2)***

4. i) Sifa za uongo – Mtemi Bokono anasifiwa kiuongo na akina Batu.

ii) Tuzo kuwaridhisha marafiki na vibaraka mf. Mtoto wa mama Kaloo alipewa kazi, Gege kupewa ardhi

iii) Kuwatenganisha wananchi wasiungane mf. kuvunjilia mbali maandamano pale Kisima cha Mkoma

iv) Ukachero na upelelezi mf. Mweke, Talui, Batu na Gege nduguye Mwelusi.

v) Matumizi ya askari – Mwelusi anateswa na kufungwa gerezani, chakula cha Mwelusi kuliwa na askari gerezani.

vi) Ukatli – kupigwa kwa wafungwa – mf. Mtuhumiwa msituni, Mwelusi, Andua na mwanawe Chendeke.

vii) Mauaji – Mwelusi aliuawa, Mtuhumiwa pia.

viii) Ushawishi unaolenga manufaa ya kibinafsi – Gege anadanganywa kwamba atapewa bintiye Bokono awe mkewe.

ix) Propaganda/uongo maji ya kisima ni ya wananchi ilhali hawayapati kila siku/kuwekea kiza kijacho, Mtemi anapenda watoto ilhali uwanja umenyakuliwa.

x) Ufisadi – kupatia vibarakala "zawadi" mf kazi kwa mtoto wa Kaloo, ama ule uwanja wa kuchezea watoto katika kijiji cha akina mama Agoro uliopewa Askari Mkuu.

xi) Sheria kali →kuzuia wananchi kunywa maji kila siku, kukutana kwa uhuru.

xii) Vitisho na uoga – Andua kupigwa na askari, kushikwa kifua
- Mwanawe Chendeke kung'olewa meno.

xiii) Tuhuma – Mwelusi kuambiwa ndiye kiongozi wa kabakaba
- Watu kudhaniwa wana makosa mf. Mtuhumiwa

xiv) Kugonganisha jamii tofauti mf. Balusi na Batuitui.

xv) Matumizi mabaya ya Baraza la Hukumu kwa kufanya maamuzi yaliyopendelea uongozi wa Bokono mf. Kanuni za kisima.

xvi) Mapuuza – Bokono kupuuza malalamishi ya wanabutangi mf. Mama Agoro

xvii) Kutia kizuizini/gerezani – Mwelusi analindwa na askari asitoroke.

xviii) Kuhini Mbutwe kutolipwa kwa viti alivyotengeneza ati mbao ni za Butangi

xix) Kuundwa kwa tume za kupumbaza Butangi kuwa matatizo yao yanashughulikiwa.

5. (i) Kinaya

i) Ni matumizi ya maneno au kauli kuelezea kitu au jambo kwa kumaanisha kingine. Yaani maneno huchukua maana na mwelekeo kinyume na mantiki au matumizi ya kawaida ya lugha.

Ifuatayo ni **mifano** ya matumizi ya kinaya katika tamthilia ya **Kifo Kisimani:**

ii) Sifa anazolimbikiziwa Mtemi Bokono ni kinaya kwa sababu anatajwa kama mpenda amani, mpenda watoto, mwenye busara, ilhali ni kiongozi mdhalimu, mfisadi na asiyejali maslahi ya raia.

iii) Ni kinaya kwa Mtemi Bokono kuuliza kama mfungwa Mwelusi aliikata minyororo kwa meno au kucha. Chuma hakiwezi kukatwa kwa meno au kucha – hukatwa kwa tupa au msumeno au kifaa cha kukatia vyuma.

iv) Gege ambaye awali hakupatana na ndugu yake Mwelusi baadaye anamwendea mama yao na kudai eti amebadilika na kuwa anampenda Mwelusi na angependa kumuomba msamaha na kumpa pole. Hiki ni kinaya kwa sababu Gege alikuwa anatafuta njia ya kumfikia Mwelusi ili amwangamize.

Powered By: www.manyamfranchise.com

v) Ni kinaya kwake Batu kusema kuwa ni rafiki yake Tanya wa tangu jadi na kuwa amemwendea ili wasaidiane. Ukweli ni kwamba alichotaka ni namna ya kumfikia Mwelusi ili aadhibiwe na utawala wa Bokono.

vi) Sifa anazojilimbikizia mwenyewe- Ni kinaya Bokono kudai anapendwa na wote ilhali mkutano wake unasusiwa na watu.

vii) Ni kinaya Zigu kusema anamtafuta Mwelusi lakini wanapokutana naye pale kisimani hamjui na hata anamuulizia.

Maelezo ya kinaya alama 2
mifano yoyote iliyoelezewa vizuri

(Hoja zozote 5x2=10)

Uongozi wa Bokono ati ni wa manufaa kwa wote ilhali ni kwa manufaa ya rafiki zake

i) na aila yake;

ii) Ni kinaya Bokono kujitia ujasiri baada ya ndoto za kutisha ilhali alikuwa na wasiwasi.

iii) Ni kinaya Bokono kudai ni mvumilivu ilhali Mwelusi anapotoroka gerezani anatishia kuitafuna mifupa ya kina Batu iwapo Mwelusi hatapatikana haraka.

(ii) Ucheshi

Ni matumizi ya lugha ambayo kwayo msanii huichekesha hadhira yake
Hutumiwa kupitisha ujumbe mkali kwa njia nyepesi.
Pia hutumiwa kuwafurahisha wasomaji.
Wasanii wengine huitumia kuondoa uchovu kwa hadhira.
Aidha pana wale ambao huitumia ili kukejeli
Huweza kusababishwa na hali si maneno tu.

Mwandishi wa tamthilia ya Kifo Kisimani ametumia ucheshi ifuatavyo:

— Kauli za Bokono katika mazungumzo na mkewe katika onyesho la pili ni za kuchekesha hasa anapoulilza "Sili? Kwani nafanya nini? Napika? Halafu anapojibu: " Alaa! Unatake kuwa mshairi .... 'jifunze mbinu zaidi za kishairi
Tashbihi pekee haitoshi (Asidondoe bali atoe maelezo)

— Gege anapodai mbele ya Bokono atimiziwe ahadi ya kuozwa Binti wa Mtemi, waliomwahidi ambao ni Batu na Mweke wanamwambia kuwa pengine ni mlevi au anaota. Hali hii ni ya kuchekesha.

— Matusi anayotoa Askari III: ni ya kuchekesha
Anasema:" Shenzi! Ningekuharibu sura kabisa. Baradhuli Mkubwa!
Yonda! Mburukenge kikongwe! Kombamwiko! ...

— Kauli ifuatayo ya Askari III vilevile inachekesha:" Umemwona ng'ombe akivuta kiko? au umemwona mbwa mwenye pembe?"

- Maelezo ya ucheshi – (alama 2)
- Mifano yoyote 5 ya ucheshi iliyoelezwa vizuri x 2 =10

6. (i) Ndoa za lazima
Wasichana waliozwa kwa lazima bila kushauriwa – Zena, Naseko.

(ii) Ndoa za mapema

- Wanawake, katika jamii ya Zena hawakudiriki kuendelea na masomo baada ya darasa la nne au tano, baadhi yao waliolewa.

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Wasichana kama Naseko wanaozwa wakiwa wadogo na kuwa vyombo vya kuzalisha watoto, wanakabiliwa na hatari ya kufa.

(iii) kutoclimishwa hadi kiwango cha juu

- Mzee Mengo kumwoza bintiye angali masomoni kunamnyima binti huyo elimu/kukatiziwa masomo.
- Zena anaolewa baada ya kukamilisha elimu ya msingi akakosa kujiunga na shule ya upili.

(iv) Kuvumilia bughudha

- Malalamiko ya Zena kuhusu dhuluma za mumewe hayakusaidia hakuweza kwenda kwao kwani alilazimika kuvumilia bughudha za mumewe – kupigwa na kutukanwa.

(v) Jamii kutarajia uvumilivu.

- Mamake Zena alivumilia taabu akaishi na mumewe; hivyo alitarajia Zena avumilie dhiki za ndoa kwa matumaini kwamba mambo yangemwongokea baadaye.

(vi) Uongozi/Ubunge

- Wafuasi wa Zena walikuwa wachache, aila yake, kutokana na mfumo wa jamii usioruhusu wanawake kujihusisha na siasa.
- Jamii imesheheni mtazamo mbaya kwa wanawake – mabango yake kuandikwa matusi.

(vii) Mavazi

- Wakati wa kampeni, ilimbidi Zena kuvalia alivyotarajiwa na jamii kwa kujitanda buibui – kitamaduni.

(viii) Masimango

- Masimango ya wanawake wenziwe yanadhihirisha jinsi taasubi ya kiume ilivyosheheni katika jamii – kwa nini apiganie ubunge hofu ya kutwaliwa waume zao na Zena, kuonyesha ni kasoro mwanamke kuishi bila mume.
- Wanawake wanaomsimanga Naseko wanadhihirisha jinsi dhuluma dhidi yao inavyohifadhiwa na kuendelezwa nao wenyewe, wameshehenewa taasubi za kiume kiasi cha kuwa wahafidhina wazo.

(ix) Kuitwa malaya

- Zena kuitwa malaya anapopigania ubunge ili wamvunje moyo kwa sababu ni mwanamke aliyetalikiwa. Uwanja wa siasa ulionekana kuwa wa wanaume pekee.
- Walioendelea na masomo waliitwa Malaya au makafiri

(x) Kuwajibu wanaume

- Mwanamke hapaswi kujibizana na wanaume, bali anapaswa anyamaze — Kisa cha Abdala.

(xi) Taasubi za Kiume

- Kushindwa kwa Zena uchaguzini kunaashiria athari za mfumo wa kuumeni usioruhusu wanawake kupigania ubunge.

(xii) Kuvunjika kwa ndoa

- Ndoa ya Zena inapovunjika analaumiwa na wanajamii kwa kutokuwa na uvumilivu.

(xiii) Kutopata watoto/kupata watoto

- Zena anapokosa kupata mtoto katika ndoa na Ali, jamii inamlaumu kwa hili.
- Mzee Sakaja - wanawake wa kumzalia watoto

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Bi Ngunga, mkewe Sakaja - alilaumiwa kwa kupata mtoto mmoja tu.

(xiv) Kuachishwa kazi.
- Mavitu amwachisha Sakina kazi ya ajira ili ashughulikea shamba → Hakuona faida yoyote ya wote wawili kufanya kazi.

(xv) Kudhibitiwa
- Sakina alidhibitiwa na mumewe ili asiandamwe na wanaume wengine – amenyimwa uhuru wa kujiamulia mambo

(xvi) Ngome ya mume
Sakina anaishi ndani ya 'ngome' ya mumewe hadi mume anapofariki ndipo anatambua umuhimu wa elimu.

(xvii) Chombo cha starehe
Mwanamke anatumiwa kama chombo cha starehe bintiye Mavitu kupachikwa mimba na jirani.

(xviii) Kutoshirikishwa
- Bi Kija hana uwezo wa kupinga maamuzi ya mumewe wala hashirikishwi.

(xix) Kutoona kosa
- Wanawake wanaompokea Naseko kwa Mzee Sakaja wanaendeleza kifungo chao kwani hawaoni kosa lolote kuozwa kwa mtoto wa shule

(xx) Mahari
- Watoto wa kike kuchukuliwa kama njia mojawapo ya kujitajirisha kwa mahari iliyolipwa mf. Naseko.

(xxi) Utawala
- Chifu kupuuza ubakaji unapotendeka

(xxii) Kupigwa
- Jamii kuchukulia kama jambo la kawaida kwa wanawake kupigwa hadi wengine wakafa mf. Mke wa pili wa Sakaja na Zena.

(xxiii) Mahali pa mwanamke
- Mtazamo kwamba mahali pa mwanamke ni jikoni – Naseko na Zena wanakatiziwa masomo ili wakaozwe na kubaki nyumbani Sakina anaachishwa kazi ili akakae nyumbani

(Hoja zozote 10 x 2 = 20)

7. (a) Hiki ni kipera cha fasihi simulizi kinachohusisha mazungumzo yenye lengo la kuhimiza mwelekeo na tabia zinazokubalika katika jamii. ***(Alama)***

(b) **<u>Muundo wa mawaidha</u>**

Mawaidha yanaweza kujisimamia au yakaegemezwa kwenye utanzu mwingine km utambaji. Yakiwa yamejisimamia, muundo wake utakuwa ufuatao:
(kuitayarisha hadhira kujua nini kunachofuata)

Powered By: www.manyamfranchise.com

→ Utangiulizi: Hapa anayetoa mawaidha huanza kwa kutoa kauli za kivutia nadhari za hadhira yake 'km "Naomba mnisikilize kwa makini nk
Uvutaja wa nadhari unaweza kuhusisha utoaji wa kiini cha mawaidha hayo km "Ni muhimu kwa kila kijana na mwanajamii kujua wajibu wake.

→ **Mwendelezo/Uwasilishaji**
Katika sehemu hii mtoa mawaidha hukazia lengo la mawaidha yake kwa kutumia mambo kama vile udondoaji wa semi au kauli za watu maarufu katika jamii. Lugha fasaha na yenye vinawirisho, viziada lugha, mabadiliko ya kasi ya mazungumzo, kupanda na kushuka kwa sauti, kimya nk. Mtoa mawaidha huusia, huonya, huelimisha kutegemea lengo la mawaidha yake.

→ **Hitimisho:**

i) **Mwasilishaji**:Aghalabu katika sehemu hii mtoa mawaidha hushirikisha hadhira yake kwa kutaka kusikia msimamo wao kuhusu mawaidha yake.
Hali kadhalika humtaka kila mmoja kuchukua hatua.
Anaweza kuwaomba kueleza ni hatua gani watachukua au kuwasisisitizia umuhimu wa kuchukua hatua huku akitumaini kuwa kila mmoja atafanya hivyo.

ii) Hadhira – maoni yao, mapendekezo yao, changamoto.

(4x1= 4)

(c) Sifa za mawaidha

i) Huhusisha kundi maalum la wanajamii (watoaji – wapokeaji)
ii) Aghalabu mawaidha hutolewa na wazee wanaochukuliwa kuwa na hekima
iii) Hutolewa kwa wadogo, vijana au watu wanaohitaji ushauri
iv) Watoa mawaidha hutarajiwa kuwa watu wenye haiba, heshima , waadilifu, wajuzi wa mambo na wenye tajriba kuu katika maisha.
v) Hutolewa katika mikutadha maalum aghalabu katika hafla/sherehe/miviga, arusi, vikao vya jamaa/familia au pahala popote ambapo yanahitajika.
vi) Tamathali za semi zinazaovuta nadhari hutumika kwa wingi.
vii) Hutumia lugha ya kipekee inayoshirikisha maneno yenye maana nzito na inayolenga kuathiri wanaousiwa.
viii) Huweza kugusia mambo mengi maishani kama vile elimu, rasilmali, maadili, urithi, mapenzi na unyumba, dini, kifo, malezi, uongozi nk.
ix) Hutofautiana kutengemea jinsia inayohusika. Mawaidha yanayotolewa kwa wavulana huweza kuwa tofauti na yale yanayotolewa kwa wasichana.
x) Viziada lugha kama vile kupanda na kushuka kwa sauti, miondoko ya viungo n.k hutumika kwa wingi.
xi) Huweza kufungamanishwa na visa maalum vilivyotokea katika jamii kusistiza ujumbe.

(Zozote 7 x 2 = alama 14)

Powered By: www.manyamfranchise.com